

## MSAADA WA KISHERIA

Ili kuepuka migongano na migogoro wakati wa ugawaji mirathi wananchi wanashauriwa kuandika wosia kwa kuwa wosia unatoa fursa kwa mtu kugawa mali yake aliyochuma kwa jinsi ambayo yeye binafsi anaona inafaa.

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

Kwa Maoni, wasiliana na Tume  
kupitia anuani ifuatayo :

Katibu Mtendaji,  
Tume ya kurekebisha Sheria  
Tanzania ,

Jengo la Taaluma Na. 1,  
Barabara ya Mkalama  
S.L. P 1718  
DODOMA  
TANZANIA

Barua pepe: [lrct@lrct.go.tz](mailto:lrct@lrct.go.tz)  
Tovuti: [www.lrct.go.tz](http://www.lrct.go.tz)



### SHERIA YA MIRATHI



#### 1.0UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kutathmini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Aidha, Tume ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma.

#### 2.0URITHI

Urithi ni mali na madeni aliyocha mtu baada ya kifo

#### 3.0SHERIA ZINAZOSIMAMIA MIRATHI TANZANIA

Lengo kubwa la Sheria za mirathi ni kuweka utaratibu wa kuhakikisha mali na madeni yaliyoachwa na marehemu yanaasimamiwa kwa kufuata taratibu ili kuepuka uwezekano wa kuhatarisha amani au kusababisha hasara kwa warithi na wadeni wa marehemu. .

Sheria zinazosimamia mirathi Tanzania ni:-

- Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Sura
- Sheria ya Mahakama za Mahakimu
- Sheria ya Mirathi ya India
- Sheria za Kiislam
- Sheria za Kimila

#### 4.0MAHAKAMA ZENYE MAMLAKA KUSIKILIZA MASHAURI YA MIRATHI

Mahakama zenye mamlaka ya kusikiliza mashauri ya mirathi ni;

- Mahakama Kuu
- Mahakama ya Wilaya kwa hakimu aliyekasimishwa mamlaka na Jaji Mkuu.
- Mahakama ya Mwanzo kwa mirathi ya kiislamu na ya kimila.

#### 5.0UTARATIBU WA KUOMBA USIMAMIZI WA MIRATHI

Ili kufungua mirathi mwombaji anatakiwa kupeleka maombi rasmi mahakamani ya kuomba kuteuliwa au kuthibitishwa (pale ambapo ametajwa katika wosia) kuwa msimamizi wa mirathi. Katika kutekeleza hili muombaji anatakiwa

kujaza fomu maalum ijulikanayo kama Fomu Na.1. Sambamba na fomu hii mwombaji ataambatisha nakala ya cheti cha kifo cha marehemu; na muhtasari wa kikao cha familia/ukoo.

#### 6.0 SIFA ZA MSIMAMIZI WA MIRATHI

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, mtu yeyote mwenye nia anaweza kuteuliwa na mahakama kuwa msimamizi wa mirathi, iwapo atakuwa na sifa zifuatazo;

- Awe mtu mzima.
- Awe na akili timamu.
- Awe mwaminifu na mwenye uwezo wa kutunza hesabu na kugawa mali za marehemu.

#### 7.0 PINGAMIZI KATIKA MIRATHI

Mtu yeyote anaweza kupeleka mahakamani pingamizi katika shauri la mirathi iwapo

hajaridhishwa na masuala yafuatavyo;

- Pingamizi dhidi ya mwombaji;
- Pingamizi la orodha ya mali za marehemu; na
- Pingamizi la mgawanyo wa mali.

#### 8.0 WAJIBU WA MSIMAMIZI WA MIRATHI

Baada ya kuteuliwa na mahakama msimamizi wa mirathi ana wajibu wa kutekeleza masuala yafuatavyo;

- kukusanya mali za marehemu;
- kusimamia kwa uadilifu na uaminifu mali za marehemu;
- kulipa madeni;
- kugawa mali hizo kwa warithi na wanufaika wa mirathi ya marehemu

#### 9.0 WAJIBU WA MSIMAMIZI WA MIRATHI

Baada ya kuteuliwa na mahakama msimamizi wa mirathi ana wajibu wa kutekeleza masuala yafuatavyo;

- Kushtaki kuhusiana na masuala yote yanayohusu mali za marehemu;
- Kudai madeni ya marehemu;
- Kuuza mali zinazohamishika ambazo zingeweza kurithiwa na mtu mwingine au mali iliyo katika shirika atakavyoona inafaa;
- Kutumia fedha kwa ajili ya kutunza na kuangalia mali; na
- Kulipia gharama za mazishi ya marehemu.

#### 10.0 HITIMISHO

Uteuzi wa Msimamizi wa Mirathi na Mahakama haumpi msimamizi huyo haki au uhalali wa kumiliki au kutumia mali za marehemu kwa maslahi yake binafsi.